


Mu komalishe, mu pangiliye, mu fanye kazi yenu ya lazima sana kwa msaada wa GMS PFCIGL, mkono inayo saidia bachuruzi kuuendelea na viwanda vidogo na via kadiri vina tumikia ku mupaka

Kikaratasi kia Projet

## Kutambulisha Usimamizi ya Mecanisme ya Msaada ao ya kuunga mkono

Mecanisme ya Kuunga Mkono (GMS) ni **mupango ya muda murefu ina tokea ku Gouvernement ya inchi ya Congo yenye iko na tumika mu cadre ya Projet ya ku rekebisha buchuruzi na kuungana ao kuunganisha batu ba mu Region des Grands Lacs ( PCFGIL) kwa msaada ya Banque Mondiale**.

Hii GMS ina ongozewa na Unite ya Usimamizi wa Projet (UGP-PFCGL) yenye ina tokea ku Ministere ya Commerce Exterieur ao Biashara ya Kimataifa na ku saidiwa na kundi ya bataalamu benye kujulikana ku jina ya **Kivu Entrepreneurs (KE) – Deloitte**. Hii muungano ya kufanya kazi pamoya ndio ina shimika mupango nyororo, na kanuni za nguvu na yenye kuwa wazi juu ya ku chagula na ku fanyisha makazi za ku sindikiza ao ku shika mkono na usimamizi wa mecanisme ya ku unga mkono ao msaada.
GMS ina tafutisha ku tia nguvu mu muungano ya **kiuchumi, ku boresha matokeo ya kazi za chaines des valeurs za ulimaji, na ku shika mkono buchuruzi yenye inafanyikaka ku mupaka na buchuruzi yenyewe ya ku nyoroka na yenye inaweza dumu muda murefu**, ku pitia ku boresha ma soko na ku patia ufahamu ao ku fundisha bikundi ya bachuruzi ba ku mupaka piya ma cooperative zenye zina fanya kazi ya ku tengeneza machakula ziki tumia mazawo ya shamba mu ma zones za mipaka zenye zili onekana kuwa za lazima zaidi .

## Lengo za projet ama vitu Projet ina taka ku fikilia

Kwa ki pekee, Projet iko na ma lengo matatu makubwa :

- **Ku shika mkono batu benye ku tumika mu ma chaines de valeurs zenye zili chaguliwa ,** benye bana onesha uwezo wa ku komala ao ku endelea na ku uzisha bitu yabo inje ya inchi ao ku vuka mupaka na ile bitu , kwa namna ya pekee ma kundi za ku simamiwa na banamuke na vijana juu ya ku patia mazawo ya shamba valeur zaidi ;
- **Ku kokota ao ku vuta ma investissements katika ma projets makubwa na za muda murefu** zenye zina saidia ku pandisha na ku ongeza mazawo ya mulimo na qualite yayo, ku pandisha niveau ya technologia, ku fanya umbalimbali na ku unda makazi zenye zina weza dumu ;
- **Ku fundisha batu ku juwa zaidi buchuruzi ya nyumbani na kuchuruziana na ma inchi jirani katika region yote** ku pitia musaada ya kiufundi( ku fundisha batu) na ku ba unga mkono kipesa.

## Mahali ao fasi projet ita fanyia kazi

GMS ina fanya kazi ndani ya jimbo la Sud-Kivu, hasa zaidi fasi zote kuna fanyiwa buchuruzi ya ku mupaka ya inchi mbili

Uvira | Sange | Luvungi | Kamanyola | Kiliba | Bukavu | Idjwi

## Projet ina husu nani ?



ACT/PCT

**Bachuruzi ba ngazi ya chini ba ku mupaka (ACT/PCT): makundi za bale** ba petits commerçants kama vile banamuke na vijana benye bana churuzaka matunda ao mazawo ya shamba mu ma chaînes de valeur zenye zina tafutiwa na kupatikana ku mupaka na ku pewa msaada ya PFCIGL.



Coopératives des agripreneurs

**Ma associations na ma coopératives ya bachuruza mazawo za mulimo:** Bikundi bienye bilisha shimikiwa ao bienye bikingali na ji shimika bienye biko ndani banamuke na vijana benye bana fanya kazi ya ku tengeneza machakula ku ngazi ya chini na benye bana uzisha inje ya mipaka mazowo za mulimo na benye banaonesha uwezo ya ku ji panga vizuri mu zile ma chaînes de valeur projet ina patia msaada.

Prestataires de services

**Batu benye bana pana ma kazi za ki uchumi :** Ma entreprises ao bikundi zenye ku boresha kazi za buchuruzi mu ma zones za ku mupaka hasa benye biko mu transport, logistique ao ma services zingine za msingi ku chaîne d'approvisionnement.

## Nani ana weza faidika na hii Projet ?

Kwa ku faidika na hii projet, lazma mutu aeneze vitu tuna taja hapa chini: :

ACT/PCT

- **Ku wa association ama kikundi cha bachuruzi ba ku mupaka benye bana kubaliwa kisheria kama bachuruzi badogo (** fasi ya kazi na kazi yenyewe bime isha chunguzwa ao ku hakikishiwa)
- **Ku tambuliwa kama ACT yenye ili andikiwa ku Ministere ya Commerce Exterieur** (ku onesha bitambulisho ao vikaratasi uli pewa na Leta)
- **Yafaa ukuwe uli onekana mu taswira ao carte mupya ya ma** ACT/P-ACT
- **Association ina pashwa kuwa iko tangu miaka mbili ,** lakini associations za mupya nazo zina kubaliwa
- **Kuwa na pesa ya buchuruzi yenye haiko chini ya 3 000 US**D yenye uli hakikisha siku bali fanya taswira ao cartographie mupya
- **Kuwa association mwanamemba wa P-ACT na ku lipa mchango wako**. Kuwa piya na wanamemba ao ba membres benye bana lipaka mchango wabo ( ku onesha liste ya wanamemba na ku hakikisha kama ba membres bana heshimu kanuni zote za kisheria)
- **Ku onesha vikaratasi vyote na habari zote kuhusu usimamizi wa mali ao gestion** : Statuts na Règlement intérieur ba membres bali kubaliana na zenye zili tiliwa cachet ya sheia , copies za PV ama ripoti ya AG ao Mukusanyo Mkubwa ya mwaka ili isha, copies ya ripoti za kipesa, na hesabu za pesa za mwaka ili pita ao mwaka jana
- **Ku pana ombi na plan ya buchuruzi yako yenye ina wezikana mu ma** chaînes de valeur zenye zina tafutiwa

- **Kuwa kikundi , coopérative, réseau ao kundi ya bachuruzi** benye balisha ji unga pamoja kama benye ku fanya kazi ya chakula toka mu kazi ya mulimo na ufugaji , bakiwa na ba membres benye bana heshimia kanuni ( kulipa mchango yabo, bana timiza mampashwa na ku fanya kila kazi yenye ina ombewa na biko na uwezo wa ku bi hakikisha ao ku bi onesha)
- **Kuwa kikundi cha banamuke ao cha vijana benye bali ji tia pamoja sawa bachuruzi** benye bana weza kuwa na ba membres karibuni 20 na 80% ya bale ba membres ni banamuke
- **Bakuwe banakuwaka tangu miaka tatu, na bameisha fanya kazi karibuni miaka mbili** ndani ya secteur yenye ina tafutiwa na hii appel ao mwito ; ma associations za ba agri-preneurs benye biko bapya na habana experience ya kazi ha ziwezi chaguliwa .
- **Kuwa déjà muko muna fanya kazi mu kawaida ya chaînes de valeur za** mavuno ao uzalishaji pia/ao transformation, ku weka ama ku funga na ku churuza mazawo za shamba mu filiere moya yenye ina tafutiwa
- **Ku wa na pesa ya buchuruzi yenye ina anzia ku $US 10.000,00, na pesa zenye una tumia zikiwa ndogo ni $ 5000** ( hii ita hakikishiwa na vitabu viako via hesabu ya pesa na ku uzisha yako, pia compte d'exploitation ao hesabu za faida na za bitu ao mali yenye ili potea ao ku homba)
- **Ku onesha bitambulisho , vikaratasi na habati zote ku husu kazi** : kitambulisho yenye ina onesha kama Leta ina ku kubalia , na reglement yako yenye iko na cachet ya notaire, na kazalika
- **Kuwa una simama imara na ku onesha uwezo technique ao wa kiufundi na uwezo pia ya ku fanya kazi ao ku tumika mu ile secteur**
- **Ku onesha habari zote zina husu usimamizi wa mali ao gestion**, maanayake repoti ya pesa ao rapports financiers/ repoti ya gisi pesa zili ingia na kutoka miaka mbili ili pita, ripoti ya gisi muna chunguza mali ndani ya kikundi na kazalika .
- **Ku pana demande na plan ya kazi** zenye kuwezikana mu ma chaînes de valeur zenye zina tafutiwa

Coopératives des agripreneurs

Prestataires de services

- Ku **tambulisha kama kazi zina fanyika** ndani ya service
- **Ku onesha kitambulisho ao ruhusa uli pewa ku fanya kazi**
- **Bakuwe bali ku hesabu siku ya mise à jour ya cartographie** ya batu benye bana pashwa faidika na projet
- Ku hakikisha kama **uko na ma equipement ao vyombo** kama vile mashini, gari za ku beba bitu , mashini za ku zalisha na zaku funga ao ku fanya emballage, ku kusanya, ku chambuwa ma produits ao mavuno, na ma services zenye una uzisha
- **Ku leta habari yenye ina husu ba clients bako, kazi zenye una fanya na programme ya makazi** na pia ripoti ya makazi za mwaka ili isha ( iki wa tayari)
- Kuwa na pesa ya kazi kwa udogo wa **$10 000** yenye uli tambulisha siku cartographie ya mupya ili fanyiwa
- Ku leta **informations ku husu uwezo wa ku tumika na usimamizi wa mali ao gestion** (vyombo via kazi, beyi ya vile vyombo, etc.)
- **Ku pana ombi na plan ya kazi zenye zina wezikana** dandi ya zile s chaînes de valeur zenye zina takiwa.

## Vitu tu na pana

**Msaada kwa njia ya technique ama ya kiufundi iko emo :**

- Ku tizama haraka na ku eleza njiya za usindikizi ao msaada tu ki simamia ku lengo za maendeleo za kila mutu mwenye ana stahili ku faidika na projet
- Ku leta mafunzo ku batu bote, na ile mafunzo yenye ina lingana na kipimo ya batu benye bana stahili faidishwa, mafunzo yenye ina saidia mwalimu na mwanafunzi ku zungumuza , ku leta mambo mapya, na ku ruhusu banafunzi pia bafundishane ao ku ongozana .
- Mafunzo ya binafsi ina letwa na mwalimu mwenye iko na bidii juu ya ku saidia mapangiliyo ya batu ku ngambo ya sheria, ngambo ya mali na ya kiufundi ao technique
- Kazi za kuunganisha makundi juu ya ku saidia ma connexion za bachuruzi na bengine benye kutumika mu chaine des valeurs, ku chochea uhusiano kati ya ma entreprise na ku boresha ku ingia ku masoko mapya mu région des Grands Lacs.

**Msaada ya kipesa yenye ina iko ndani :**

- misaada za ku tengeneza viwanda vidogo , ku nunuwa vyombo vya lazima vya msingi juu ya transformation, transport ao ku logistique na ku ma hatuwa zote juu ya ku pewa vikaratasi na kwa ku pata mafunzo yaku linganisha ufundi.
- ku saidia batu kujuwa kutumia mali juu ya ku hakikisha kama pesa zina tumiwa kufwatana na ma lengo ao ma objectifs, na uwaziwazi ya pesa zenye zita koka inje na gisi ya ku fanya ili investissement ama kwenye pesa zili tumika pa dumu

## Ngazi ao hatuwa zenye zita fwata

| Ngazi | Zone* | Muda |
|---|---|---|
| **Ku anzisha kiwazi GMS** | zone zote | 15 /08/2025 |
| **Zone A : Uvira, Sange, Luvungi, Kiliba** | | |
| **Ku ita ma candidatures – ACT na batu ya ma services** | Zone A | 1er sept - 31 oct. 2025 |
| **Ku ita ma candidatures – Coopératives** | Zone A | 1er nov. 2025 – 4 janv. 2026 |
| **Ku julisha benye bali pita – ACT na batu ya ma services** | Zone A | Janvier 2025 |
| **Ku ita benye bali pita - Coopératives** | Zone A | Mars 2026 |
| **Zone B : Bukavu, Idjwi, Kamanyola (kama hali ya usalama ina kuwa bora)** | | |
| **Ku ita ma candidatures – ACT na batu ya ku leta ma services** | Zone B | Octobre – Novembre 2025 |
| **Ku ita ma candidatures – Coopératives** | Zone B | Décembre – Janvier 2026 |
| **Ku itia benye bali pita – ACT na batu ya ku leta ma services** | Zone B | Février 2026 |
| **Ku julisha batu benye bali pita- Coopératives** | Zone B | 03 /2026 |
| **Zones zote** | | |
| **ACT et prestataires de services** | Zone zote | 05/ 2026 |
| **Coopératives** | Zone zote | 06/ 2026 |